CATHOLIC SECRETARIAT
TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE

P.O BOX 2133
PHONE 022/2851075-7-8
022/2850047
022/2850017
FAX 022/2851133; 2850427.
DOMAIN: TEC.CO.TZ
E-Mail: info@tec.or.tz
DAR ES SALAAM
TANZANIA

# TAMKO LA BARAZA LA MAASKOFU KATOLIKI TANZANIA (TEC) KUHUSU AMANI KWA TAIFA KUELEKEA SIKU YA UCHAGUZI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA UTAKAOFANYIKA TAREHE 29 OKTOBA 2025.

## *"SAUTI YA WATU, SAUTI YA MUNGU"*

## UTANGULIZI

*"Maana Kristo mwenyewe ametuletea amani kwa kuwafanya Wayahudi na watu wa mataifa mengine kuwa jamii moja. Kwa mwili wake yeye mwenyewe aliubomoa ule ukuta uliowatenganisha na kuwafanya maadui. Aliiondoa ile sheria pamoja na amri zake na kanuni zake, ili kutokana na jamii hizo mbili aumbe jamii moja mpya katika umoja naye na hivyo kuleta amani. Kwa mwili wake, Kristo aliuangamiza uadui wao; kwa msalaba wake aliziunganisha jamii hizo kuwa moja na kuzipatanisha na Mungu" (Waefeso 2:14-16).*

**Sisi Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania,**

1. Tunatambua kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na pia -

2. Tunatambua kuwa Ibara ya 5 (1) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzainia imempa haki kila raia aliyetimiza miaka kumi na minane kupiga kura. Kwa mujibu vifungu vya 81 (1) na (2) na 85 (1) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na kwa hivyo -

3. Kwa kutambua kwamba mamlaka ya Serikali inayotawala Raia wake Kidemokrasia yanatoka kwa Wananchi, sisi Maaskofu wa Kanisa Katoliki nchini Tanzania, tumetazama kwa jicho la Kimungu mambo yanayoendelea nchini hasa katika kipindi hiki muhimu cha Uchaguzi Mkuu, tumesikiliza sauti za waumini, viongozi, wananchi pamoja na wadau mbalimbali wa masuala

ya kisiasa nchini, tumesali na kutafakari kwa kina, na hivi tunatamka ifuatavyo;

3.1. Kanisa Katoliki Tanzania halijihusishi na masuala ya kisiasa lakini linawajibika kutoa mawazo, ushauri na mtazamo wake kwa waumini, wananchi na Serikali juu ya mambo muhimu yenye mustakabali wa maendeleo ya raia na Taifa.

3.2. Tunafahamu kuwa mchakato wowote wa Kidemokrassia hujumuisha michakato ya wazi, hutoa fursa ya ushiriki wa pande zote muhimu katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu ili kuepusha mivutano au machafuko katika eneo husika.

3.3. Kanisa tunao wajibu wa kuwakumbusha waumini wetu ambao ukiachilia mbali imani yao ambayo imejengwa juu ya dhehebu Katoriki lakini bado wengi wao wanashiriki katika medani za kisiasa wakiwa kama wanachama, viongozi, watumishi na waandamizi wa vyama tofautitofauti kuwasihi kulinda amani ya nchi katika shughuli zao za kila siku.

## WITO WA BARAZA LA MAASKOFU KWA WAUMINI WA KANISA KATOLIKI TANZANIA.

**Sisi Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania,**

4. Kwa kuzingatia historia na uhalisia wa athari za machafuko ya Kisiasa ambayo yamekuwa yakishika kasi katika mataifa mengine ulimwenguni, Kanisa Katoliki nchini linawasihi waumini wake na Watanzania kwa ujumla kutoshiriki, kutoratibu au kuhamasisha mipango ya uvunjifu wa amani Ili kulinda ustawi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
5. Tunatoa wito, kwa waumini, wananchi, viongozi na wadau wa siasa ambao kwa namna moja au nyingine hawajaridhishwa na mwenendo wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu nchini kutafuta njia rafiki za kuondoa changamoto wanazoziona kuliko kutumia kauli chonganishi ambazo zinaweza kuvuruga amani na taswira ya Tanzania Kitaifa na Kimataifa.
6. Tunawasihi Watanzania wote, bila kujali imani zao, chama au msimamo wao wa kisiasa, **kutojihusisha na dhamira yoyote itakayoandaliwa kwa kusudi la kuchochea maandamano,**

**ghasia za machafuko, vurugu, uharibifu wa mali za umma au binafsi nchini.**

7. Tunawahimiza wananchi, viongozi na mamlaka zote nchini kuendelea **kuheshimu haki na maoni ya wengine**, hususani wale wenye maoni tofauti kisiasa ili kudumisha mshikamano wa Kitaifa kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu Tanzania.
8. Tunawasihi watawa, viongozi wa jumuiya, Vigango na Parokia za Kanisa Katoliki Tanzania kutekeleza wito wao wa kuihubiri amani kwa mataifa yote ili kuzuia haiba ya watu wote wanaojaribu kuhamasisha fujo katika mitandao ya kijamii, maeneo ya kazi na makazi.
9. Aidha Baraza la Maaskofu Tanzania, tunatoa wito kwa kiongozi yeyote atakaeshinda nafasi ya Urais Tanzania kuliongoza Taifa, awe tayari kuliunganisha Taifa mara baada ya Uchaguzi Mkuu na kuchukua hatua madhubuti za kuendeleza amani na mshikamano kwa maendeleo ya Taifa.

**HITIMISHO:**

Kwa kuzingatia mchakato wa **Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 29 Oktoba 2025**, Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania tunathibitisha msimamo wetu wa kudumisha amani, umoja na mshikamano wa Kitaifa. Tunatoa wito kwa waumini wa Kanisa Katoliki na Watanzania wote, bila kujali chama au msimamo wa kisiasa, kuendelea kuwa walinzi wa amani, kuepuka vitendo vyote vya fujo, na kuheshimu haki na maoni ya wengine.

Baraza la Maaskofu tunasisitiza kuwa mshikamano wa kitaifa, heshima ya utu wa binadamu, na ushirikiano wa kijamii ni nguzo kuu za maendeleo ya Tanzania. Tunawahimiza viongozi, waumini, na Wananchi wote kushirikiana kikamilifu katika kulinda amani, kudumisha umoja wa Kitaifa, na kuchukua hatua za hekima katika kukabiliana na changamoto zozote zitakazojitokeza wakati na baada ya Uchaguzi.

Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania.

Ni sisi Maaskofu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania:

1. Askofu Wolfgang Pisa OFMCap - Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, na Askofu wa Lindi.
2. Askofu Eusebius Nzigilwa Makamu wa Rais wa Baraza La Maaskofu Katoliki Tanzania na Askofu wa Mpanda
3. Askofu Flavian Kassala - Askofu wa Geita
4. Askofu Mkuu Grevas Nyaisonga - Askofu Mkuu wa Mbeya
5. Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya OFNCap - Askofu Mkuu wa Dodoma
6. Askofu Mkuu Yuda Thadei Ruwa'ichi OFMCap - Askofu Mkuu wa Dar es Salaam
7. Askofu Mkuu Damian Dallu - Askofu Mkuu wa Songea
8. Askofu Mkuu Isaac Amani - Askofu Mkuu wa arusha
9. Askofu Mkuu Renatus Nkwande - Askofu Mkuu wa Mwanza
10. Mwadhama Protase Kadinali Rugambwa – Askofu Mkuu wa Tabora
11. Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa – Askofu wa Iringa
12. Askofu Michael Msonganzila – Askofu wa Musoma
13. Askofu Ludovick Minde ALCP/OSS – Askofu wa Moshi
14. Askofu Method Kiaini – Msimamizi wa Kitume wa Bukoba
15. Askofu Agapitus Ndorobo – Askofu wa Mahenge
16. Askofu Joseph Nlola ALCP/OSS – Askofu wa Kigoma
17. Askofu John Ndimbo – Askofu wa Mbinga na Msimamizi wa Kitume wa Njombe
18. Askofu Salutaris Libena – Askofu wa Ifakara
19. Askofu Almachius Rweyongeza – Askofu wa Kayanga
20. Askofu Liberatus Sangu – Askofu wa Shinyanga
21. Askofu Titus Ndoe – Askofu wa Mtwara
22. Askofu Bernadin Mfumbusa – Askofu wa Kondoa
23. Askofu Prosper Lyimo – Askofu msaidizi wa Arusha
24. Askofu Edward Mapunda – Askofu wa Singida
25. Askofu Beatus Urassa ALCP/OSS – Askofu wa Sumbawanga
26. Askofu Anthony Lagwen – Askofu wa Mbulu
27. Askofu Bilbert Nhasi – Askofu wa Tunduru Masasi
28. Askofu Lazarus Msimbe SDS – Askofu wa Morogoro
29. Askofu Simon Nasondole – Askofu wa Bunda
30. Askofu Henry Nchamungu – Askofu msaidizi wa Dar es Salaam

31. Askofu Stefano Musomba OSA – Askofu wa Bagamoyo
32. Askofu Christopher Ndizeye – Askofu wa Kahama
33. Askofu Nteule Thomas Kiangio – Askofu wa Tanga
34. Askofu Severine NiweMugizi – Askofu wa Rulenge – Ngara
35. Askofu Augustine Shao CSSp – Askofu wa Zanzibar

Imetolewa Dar es Salaam,

Tarehe 11 Oktoba ya Dominika ya 28 ya Mwaka C wa Kanisa 2025.

Mhashamu AskofuWolfgang Pisa OFCMap
Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania.

Pd. Charrles Kitima
Katibu Mkuu wa Baraza